



# Haja ya vijana kujihusisha na ulmwengu wa kazi

## Taarifa kwa wazazi na walezi

Wanafunzi wanahitaji fursa za kujifunza kutoka kwa waajiri kuhusu kazi, ajira ya kulipwa na ujuzi unaothaminiwa mahali pa kazi. Hii inatumika kwa wanafunzi wote, iwe wanatafuta kuingia moja kwa moja katika chuo kikuu, wanaonua kufanya mafunzo zaidi watakapomaliza shule, au wakiwa wanapanga kuhamia moja kwa moja kwenye nguvu kazi.

Kujihusisha na ulmwengu wa kazi huwasaidia vijana kuelewa umuhimu wa kile wanachojifunza shulen, kupanua upeo wao, kuinua matarajio yao, na kuangazia utofauti wa kazi na njia za kazi zilizo wazi kwao.

Vijana wanahitaji fursa kuweza:

- kuthibitisha kuwa wanategemewa
- kuonyesha wanajua jinsi ya kufanya kazi
- kuboresha kujiamini
- kukuza ujuzi.

Fursa za vijana kupata uzoefu wa ulmwengu wa kazi ni pamoja na:

- kazi za muda na za kawaida zisizokuwa za kudumu
- kujifunza mahali pa kazi na uzoefu wa kazi kuititia programu ya shule
- kazi ya kivuli
- kujitolea
- kutembelea mahali pa kazi
- majaribio ya kazi na mafunzo tarajali
- vilabu vya michezo
- ujasiriamali na uanzishaji biashara’.

Uzoefu huu utasaidia kujenga maarifa na ujuzi unaohitajika ili kupata na kuendeleza ajira, na kuendelea mahali pa kazi.

### Kujenga uwezo wa kufanya kazi

Uwezo wa kufanya kazi unawakilisha tabia au mitazamo inayothaminiwa zaidi, inayotambuliwa na kuthaminiwa mahali pa kazi. Waajiri wanazidi kusisitiza haja ya wafanyakazi kuwa na kuweza kuonyesha uwezo wa kazi.

Ujuzi muhimu wa kuajiriwa uliotambuliwa na Tume ya Kitaifa ya Ujuzi ni pamoja na:

- |  |   |
|--|---|
| <ul style="list-style-type: none"><li>• Ujuzi wa mahusiano mazuri na wengine na watu</li><li>• Ujuzi wa kupanga na kupangilia</li><li>• Kuegemea na motisha</li><li>• Kufikiri kwa makini na utatuzi wa matatizo</li></ul> | <ul style="list-style-type: none"><li>• Ujuzi wa mawasiliano na kazi ya pamoja</li><li>• Kubadilika na kustahimili</li><li>• Kujuua kusoma na kuandika kidijitali</li></ul> |
|--|---|

